



# SHAIRI LA UZINDUZI WA SIKU YA LISHE KITAIFA – 7 AGOSTI, 2020



1. Saba Gosti Mbili Ziro, Leo Tunaisimikaaa,  
Siku ya Lishe Wapendwa, Lazima Kusherehekaa  
Taifa Letu Ni Pendwa, Sote Tunafurahikaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
2. Wizara Yetu ya Afya, Leo Ndio Yatangazaa,  
Jamii Kuwa na Afya, Wizara Yasisitizaa,  
Mlo Kamili Ni Afya, Hili Ndilo Tunajuzwaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbu-
3. Siku hii ni ya Lishe, Sote Tumefurahishwaaa,  
Lishe, Kinga Kwetu Sote, Ndio Tunavyokumbushwaa,  
Tumeianzisha Leo, Hivi ndivyo ilipashwaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
4. Mlo ulio Kamili, Kwa Wote Yawezekanaa,  
Ndizi, Mizizi Asili, Na Nafaka Tunajuaa,  
Huleta Nguvu kwa Mwili, Nishati Inaongezaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
5. Kuleni Kunde Maini, Pia Kuleni na Nyamaa,  
Asili yake Protini, Mwili Kujenga Nasemaa,  
Popote Tutafuteni, Imara Tutasimamaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
6. Mbogamboga Za Kijani, Zahitajika Mwilinii,  
Biringanya na Bamia, Kinga Imara Tulenii,  
Ni Vyema Kuvitumia, Vizuri Tuwe Makinii,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
7. Matunda Nayayo Muhimu, Kuyatumia Kwa Sana,  
Ufyonzwaji wa Madini, Ya Chuma Hupatikanaa,  
Chungwa, Chenza Nayayo Ndimu, Magonjwa Kuepukanaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
8. Watoto wetu Wachanga, Makini Mama Nyonyeshaa,  
Miezi Sita Ya Mwanzo, Ziwa la Mama Latoshaa,  
Maziwa Haya ya Mwanzo, Mwili Huirutubishaa,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
9. Wanaume Na Wakike, Vijana Hata Wazeee,  
Lishe kwetu Itumike, Jamii Tuiongozee,  
Kwa Haya Tuelimike, Wengine Tuelekezee,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku Ya Kukumbukaa.
10. Wataalam wa Hakika, Wanapatikana Lishee,  
Kwa Dhati Wanatumika, Kwa Masuala ya Lishee,  
Jamii Ilo Tukuka, Tumieni Wana Lishee,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
11. Wamefunzwa Kwa Makini, Kuhudumia Jamii,  
Kwa Taarifa Makini, Kuzitoa kwa Jamiiii,  
Kaskazini na Kusini, Siha Njema kwa Jamii,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
12. Basi kwa Haya Yatosha, Kulikunja Jamvi Hiliii,  
Mafunzo Yamewatosha, Katika Jukwaa Hiliii,  
Niseme Pia Yatosha, Kuwashukuru kwa Hilii,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku ya Kukumbukaa.
- 13 Tamati Nimefikia, Kalamu Naweka Chinii,  
Yote Yalowafikia, Msije Yaweka Chinii,  
Na Lishe Kuwafikia, Wajuu hata wa Chinii,  
Saba Gosti Mbili Ziro, Ni Siku Ya Kukumbukaa.

**Limetungwa na Kughaniwa na Bi. Aysha Iddy Mgaya  
Idara ya Sera na Mipango ya Lishe  
Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC)**

**LISHE BORA NI KINGA THABITI  
DHIDI YA MAGONJWA**

**Imetolewa na:**

**Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania**